



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUANGWA



**TANGAZO LA NAFASI ZA WAHUDUMU WA AFYA NGAZI  
YA JAMII KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA  
RUANGWA, MKONI LINDI**

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia **Wizara ya Afya na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI)** inatekeleza **Mpango Jumuishi wa Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii** nchini. Kupitia Mpango huu, Serikali imeweka utaratibu wa kuwapata Wahudumu wenye sifa zilizowekwa, kutoa mafunzo na kuwatumia Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii katika utekelezaji wa afua Jumuishi za Afya, Lishe na Ustawi wa Jamii ambapo Mpango unahitaji Wahudumu wawili (2) yaani Mwanaume na Mwanamke kwa kila Kitongoji/Mtaa.

Katika kutekeleza Mpango huu, **Wizara ya Afya** kwa kushirikiana na **Ofisi ya Rais - TAMISEMI** inawatangazia wananchi kuwa Mpango huu kwa awamu ya kwanza umeanza kutekelezwa katika Mikoa 10 ukiwemo Mkoa wa Lindi. Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa, mkoani Lindi ni mnufaika wa Mpango huu ambapo Wahudumu wapatao 872 wanatarajiwa kuchaguliwa kutoka Vitongoji 436 vya Halmashauri hii.

Aidha, utekelezaji wa Mpango huu utaendelea kwa awamu katika Mikoa na Halmashauri zote za Tanzania Bara. Wananchi wakiwemo watu wenye ulemavu wenye sifa stahiki ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa wanahimizwa kuomba nafasi za Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii katika Vitongoji vyote. Maombi yote yawasilishwe kwa Maafisa Watendaji wa Kata, ambao watasimamia zoezi la kuwachagua Wahudumu wenye sifa miongoni mwa waliotuma maombi kwa kuzingatia Miongozo iliyotolewa.



**Sifa za waombaji:**


- a) Awe na utambulisho rasmi kama vile Kitambulisho cha Taifa (NIDA) au hati ya kusafiria au Leseni ya udereva au Kitambulisho cha mpiga kura;
- b) Awe amemaliza Elimu ya Sekondari (angalau Kidato cha Nne) na awe na Cheti cha kuhitimu (*Leaving Certificate*);
- c) Awe ni mkazi na kwa sasa anaishi Kitongoji na Mtaa husika;
- d) Awe anafahamu lugha, utamaduni, mila na desturi za jamii husika;
- e) Akubalike kimaadili na kiutamaduni na jamii husika;
- f) Asiwe na historia ya vitendo vya uhalifu ikiwemo unyanyasaji wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto;
- g) Awe na moyo wa kujituma, mchapakazi na mwenye ari ya kutumikia jamii;
- h) Awe mwaminifu na mwenye uwezo wa kuweka taarifa za mteja kuwa siri;
- i) Awe na utayari na uwezo wa kufanya kazi katika Kitongoji au Mtaa husika; na
- j) Awe na umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 55;

**Maombi yawasilishwe Ofisi ya Mtendaji wa Kata yakiambatanishwa na:**

- a) Barua ya maombi ya kazi iliyoandikwa kwa mkono na kuweka saini ya mwombaji;
- b) Nakala ya Cheti cha kuhitimu Kidato cha Nne (*Form IV leaving Certificate*);
- c) Picha mbili (2) za *Passport Size*;
- d) Maelezo binafsi (CV), ikionyesha umri, anuani kamili na namba ya simu ya kiganjani, pamoja na anuani/namba ya simu ya kiganjani ya Wadhamini wasiopungua wawili (2).
- e) Barua ya uthibitisho kutoka kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji/Mtaa wa eneo analotoka.

Mwisho wa kuwasilisha maombi haya ni siku ya Jumatatu tarehe 21 Julai, 2024. Maelekezo zaidi yanapatikana kupitia Ofisi ya Watendaji wa Kata.

Imetolewa na:

  
Frank F. Chonya  
**MKURUGENZI MTENDAJI**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA RUANGWA**